TANGAZO LA SERIKALI NA. 624 la tarehe 1/9/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))*

AMRI YA NAULI ZA MIZIGO KATIKA ZIWA VICTORIA YA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Mizigo Katika Ziwa Victoria ya Mwaka 2023 na itaanza kutumika baada ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuchapishwa.

Matumizi

2. Amri hii itatumiwa na meli zinazomilikiwa na Kampuni wakati wa kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo maeneo ya Tanzania katika Ziwa Victoria.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 415

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

Sura ya 212

"Kampuni" maana yake ni Kampuni ya Huduma za Meli iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni;

"Shirika" maana yake Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"meli" maana yake ni meli zinazoendeshwa na Kampuni katika Ziwa Victoria.

## SEHEMU YA PILI
## NAULI NA MASHARTI YANAYOTUMIKA

Nauli zilizoidhinishwa

4. Kampuni inayoendesha meli: -

(a) itatoza nauli ya mzigo isiyozidi ongezeko la asilimia 17.7 kutoka kiwango cha nauli ya mzigo kilichoidhinishwa kwa njia ya Mwanza-Bukoba;

(b) itatoza nauli ya mzigo isiyozidi ongezeko la asilimia 16.9 kutoka kiwango cha nauli ya mzigo kilichoidhinishwa kwa njia ya Mwanza-Ukerewe;

(c) itatunza taarifa za usafirishaji abiria na mizigo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo udhibiti;

(d) itazingatia masharti ya utoaji huduma ya usafiri kwa njia ya maji yaliyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini. *(Sura ya 165)*

Masharti ya huduma

5. Wakati wa kutoa huduma, Kampuni itazingatia masharti yafuatayo:

(a) itatengeneza chati za nauli za mizigo kwa kuzingatia masharti ya aya ya 4(a) na (b) na kuwasilisha chati hizo kwa Shirika ndani ya siku saba tangu kuanza kutumika kwa Amri hii;

(b) itatoa tiketi kwa abiria zinazoonesha nauli isiyozidi viwango vilivyoidhinishwa;

(c) itatoa tiketi kwa abiria wakiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;

(d) itapima uzito wa mizigo ikiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;

(e) itaimarisha mikakati ya kimasoko ili kuongeza idadi ya abiria na shehena;

(f) itazingatia ratiba ya safari za meli kama ilivyotolewa na Kampuni kwa wateja; na

Sura ya 165

(g) itazingatia viwango vya usalama kama vilivyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake.

Dar es Salaam
1st August, 2023

KAIMU ABDI MKEYENGE
*Mkurugenzi Mkuu*